

# TANGAZO

- ◆ HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE KUPITIA IDARA YA KILIMO INAWALETEA WANANCHI WOTE NJIA BORA YA KUHIFADHI MAZAO YENU BILA KUTUMIA KEMIKALI, TUMIA MIFUKO YA PICS (YENYE TABAKA TATU), MIFUKO HII INA FAIDA KIAFYA, KIUCHUMI, KIJAMII NA KIBIASHARA, INAWEZA IKATUMIKA KWA MISIMU MITATU IKITUNZWA VIZURI.
- ◆ MFUKO MMOJA UNAUZWA KWA TSHS 5,000 TU, INAPATIKANA KATIKA OFISI YA KILIMO (W) UKEREWE, FIKA NA UPATE MAELEKEZO YA NAMNA YA KUITUMIA.
- ◆ KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA AFISA MAZAO (0752526789, 0786983585).




# Mifuko Ya PICS : Hifadhi Ya Mazao Bila Kutumia Kemikali (Mifuko Ya Tabaka Tatu)



**1** Nunua mifuko halisi ya PICS kutoka kwa wauzaji waliodhinishwa/sajiliwa. Hakikisha PICS ina tabaka tatu




**2** Hakikisha mazao unayohifadhi yamekauka na ni safi (bila taka/uchafu)




**3** Chunguza mifuko miwili ya ndani isiwe imetoboka au kuchanika (usitumie mifuko iliyotoboka)




**4** Weka kiasi kidogo cha mazao katika mfuko wa kwanza na tumbukiza katika mfuko wa pili




**5** Tumbukiza mifuko yote miwili katika mfuko wa tatu wa kiroba. Kunja mifuko yote mitatu pamoja kuanzia juu



**6** Jaza mazao katika mfuko ukitikisatikisa taratibu ili mfuko ujae vizuri na kuondoa hewa. Hakikisha kunabaki nafasi kwa ajili ya kufungia mfuko




**7** Kandamiza vizuri na taratibu mfuko wa kwanza ili kuondoa hewa kisha uonyonge na kuufunga kwa kamba. Fanya vile vile kwa mfuko wa pili na wa tatu



**8** Hatua ya 1 : Funga mfuko wa kwanza ndani  
Hatua ya 2: Funga mfuko wa pili wa kati  
Hatua ya 3: Funga mfuko wa tatu wa nje

## Unashauriwa:

- ✓ Usihifadhi mifuko ya PICS juani au kwenye joto kali
- ✓ Usiweke mifuko chini sakafuni, weka mifuko juu ya boriti / mbao/magogo
- ✓ Usiegеше mifuko ya PICS katika ukuta ili kuruhusu kuikagua mara kwa mara
- ✓ Usitunze mifuko ya PICS sehemu moja na mifuko mingine iliyo na mazao yaliyoshambuliwa na wadudu



*"Mifuko ya PICS - inaboresha thamani ya mazao nakuongeza uhakika wa chakula"*

### CONTACT:

Purdue Improved Crop Storage  
Department of Entomology  
Purdue University  
West Lafayette, IN 47907  
Email: picinfo@purdue.edu  
Phone: +1-765-494-4554

Peet Pee (Tanzania) Limited  
Kange Industrial Area  
New Korogwe Road,  
Plot no. 2, 3, 4  
P.O. Box 34  
Tanga, Tanzania, East Africa

Contact Person:  
Mr. Thompson Mwakibinga  
PICS Commercial Manager (PPTL)  
Mob: +255-784-871-902, +255-765-261-150  
Email: thompson@pptl.biz

Email: sales@pptl.biz  
support@pptl.biz  
Phone: +255-27-264-68534  
+255-27-264-7519  
Fax: +255-27-264-6882

Mr. Laddatus Ng'ingo  
PICS Project Manager (PPTL)  
Mob: +255-784-740-650, +255-716-162-949  
Email: ngingo@pptl.biz

Usanifu : D. Banburtsa, I. Baoua, T. Abdoulaye, C. Dabiré, C. Alexander & L. Murdock  
Michoro : Boukari Mamadou, Niger

**PURDUE**  
UNIVERSITY

